**MTIHANI WA MWIGO WA CEKENAS – 2016**
**KISWAHILI**
**INSHA**
**102/1**
**KARATASI LA KWANZA**

1. Mwandikie mhariri wa gazeti la 'Tujuze' ukilalamikia swala la uharibu wa mazingira katika eneo unakoishi na jinsi ya kukabiliana na changamoto hii.
2. Mitandao ya kijamii imesababisha madhara mengi katika sekta ya elimu. Fafanua.
3. Mcha mwana kulia, hulia mwenyewe.
4. "Buum!" Mlipuko huo ulitapakaza vifusi kote. Nilijua lazima ningejinusuru ....... Iendeleze insha hii.

**MTIHANI WA MWIGO WA CEKENAS – 2016**
**KISWAHILI**
**102/2**
**LUGHA**
**KARATASI LA PILI**

1. **UFAHAMU (alama 15)**

**Soma makala ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatia.**

Utandaridhi (au globalization kwa lugha ya Kingereza) ni jinsi ya maisha inayoendelea kuutawala ulimwenguni wote katika karne hii ya 21. Neno utandaridhi ni neno mseto ambalo maana yake ni utamaduni uliotanda au kuenea ardhi nzima. Mtu mtandaridhi hivyo basi ni mtu aliyebobea kikamilifu katika utamaduni huu mpya kwa jinsi moja au nyingine. Mtandaridhi hujihusisha sana katika kutandaridhisha aina moja au nyingine ya amana muhimu za mavazi zilizotokea kupendwa ulimwenguni kote, muziki wa kisiku hizi, hasa vile op, raggae, ragga, rap, ambao asili yake ya hivi majuzi ni Marekani. Muziki huo waimbaji wake hutumia, sana sana, lugha ya Kingereza hususan kile cha Marekani na kadhalika.

Watandaridhi wana nyenzo zingine kadha wa kadha za kuendeshea maisha yao au kujitambulisha. Wao huwasiliana kutoka pembe moja ya dunia hadi nyingine wakitumi vitumeme, yaani vyombo vitumiavyo umeme kufanya kazi vya hali ya juu, kama vile tarakilishi na simu, haa za mkono. Watu hawa hawakosi runinga sebuleni mwao, usiseme redio. Hawa husikiliza na kutazama habari za kimataifa hupitia mashirika matandaridhi ya habari kama vile BBC la Uingereza na CNN la Marekani. Aidha watu hawa husafiri mara kwa mara kwa ndege na vyombo vingine vya kasi. Hawa hawana mipaka, wote wanaohusudu utandaridhi wanaamini kindakindakika kwamba utamaduni huu ni kilimwengu umeleta miahaka mwema baina ya watu binafsi, makampuni makubwa makubwa ya kimataifa na uwiano bora baina ya mataifa. Watu hawa husikika wakidai ya kuwa aina hii ya utamaduni imeupigisha mbele ustaarabu wa wanadamu ulimwenguni kote. Kwa upande mwingine, wakereketwa wa tamaduni za kimsingi za mataifa na makabila mbalimbali ulimwenguni wanadai ya kwamba utandaridhi umeleta maangamizi makubwa ya tamaduni hizo. Vile vile unaelekea kuangamiza lugha nyingi zinazofungamana na tamaduni hizo.

Kwa ajili hiyo basi, utandaridhi umesemekana kwamba unasababisha kutovuka kwa utu miongoni mwa wanadamu wote ambao wamo mbioni kusaka pesa na kuneemesha ubinafsi. Inadaiwa pia kwamba utandaridhi umesababisha kutovuka kwa adabu kwa vijana wengi ulimwenguni kote ghaya ya utovu. Huko kutovuka kwa adau kwa vijana, hasa wale wa mataifa yanayojaribu kuendelea, kumeleta zahama chungu mbovu, ikiwa ni pamoja na kuenea kwa UKIMWI kwa kasi ya kutisha.

**Maswali**

(a) (i) Bainisha kwa kutoa maelezo kamili kwamba utandaridhi ni neno mseto. (alama 2)
(ii) Tohoa maneno mawili kutokan ana neno kutandaridhisha kisha ueleze maana ya maneno haya. (alama 4)
(b) Ni nini maana ya "hawa hawana mipaka"? (alama 1)
(c) Kwa nini watandaridhi wanapenda kusikiliza na kutazama habari kupitia BBC na CNN? (alama 2)
(d) Eleza kikamilifu maoni ya watandaridhi kuhusu utamaduni wao. (alama 2)
(e) Je, utandaridhi unalaumika kwa nini katika kifungu hiki? (alama 2)
(f) Msemo: "Chungu mbovu" ni msemo wa kimtaani tu. Msemo swa ni upi? (alama 1)

2. **MUHTASARI (alama 15)**

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali.**

Kiswahili lugha yenye asili yake katika ukanda wa Afrika Mashariki imeenea duniani ambako inafundishwa katika uyuo vikuu saba vya umma na vyuo vikuu viwili visivyo vya umma. Hivi ni Baratoni na Chuo kikuu ch aKikatoliki. Katika kiwango hiki, watu wanafunzwa isimu na fasihi mafunzo haya yanatolewa kuanzia shahada ya kwanza, shahada ya uzamili na shahada ya uzamifu.

Elimu ya juu ya Kiswahili inatiliwa mkazo katika vyuo vikuu nchini Tanzania na hasa Dar-es-Salaam. Chuo hiki ndicho mlezi wa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI). Kwa muda mrefu, TUKI imechapisha mararida, kuzua istilahi na kuandaa kamusi. Vyuo vikuu nchini Uganda vikiongozwa na Makerere vimeanzisha mikakati kabambe ya kufunza Kiswahili. Kwingineko barani Afrika, Kiswahili kinafunzwa nchini Msumbiji, Sudan, Misri, Lesotho, Ghana, Nigeria n.k

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

lugha hii imepewa msisimko mkubwa katika mitaala kuambatana na sera ya Afrika Kusini kutukuza lugha za Kiafrika. Ikumbukwe kuwa lugha hii ilichangia pakubwa ukombozi wa Afrika Kusini.

Ukitembelea baadhi ya vyuo vikuu katika nchi za mashariki ya mbali kama Japani, Kora Kusini na Uchina, utapata Kiswahili kwenye orodha ya masomo. Maandishi mengi yanatafsiriwa kwa Kiswahili katika vyuo hivi. Takribani nchi zote ulaya zina vyuo vikuu vinavyofunza Kiswahili. Lakini Uingereza, Ujeremani na nchi za Skandinevia zimetia fora, pamoja na kufunza lugha hii, vyuo vinafadhili utafiti na uchapishaji wa mambo kuhusu Kiswahili. aidha nchi hizo huwadhamini wengi kusomea huko. Muhimu zaidi ni kuwa vyuo vikuu katika nchi hizo zimehifadh maandishi mengi ya Kiswahili. Hivi sasa masomo mengi wanayatumia kufanya utafiti hasa hukusu ushairi. Moja ya asasi hizi ni School of Oriental and African studies. Jijini London. Wataalamu waliosomea vyuo hivi wamerudi nyumbani na sasa wanajihusisha na uchapishaji wa vitabu vya nadharia, isimu, surufi, fasihi andishi na fasihi simulizi.

Hata hivyo, ni Marekani ambapo matumizi na mafunzo ya Kiswahili katika vyuo vikuu yamepanuka sana. Lugha hii inafunzwa katika majimbo kama Washington, New York, Chicago, Texas, California, New Jersey n.k. vyuo maarufu sana vile Cornel, Yale na Havard vinafunza Kiswahili. Hali hii imesaidia kuingizwa kwa lugha hii katika mtandao.

Lugha hii inafunzwa kama ishara ya hisia za Uafrika. Wamerekani weusi wanaona fahari kuzungumza Kiswahili. Hii huwakumbusha kuwa wao wana asili ya barani Afrika. Kupitia mafunzo haya, Wamerekani wengi wanaiga utamaduni wa Kiafrika. Wengi wao wamejipa majina ya Kiswahili kama vile Baruti Katembo Maulana, Simba n.k. kwa hakika Kiswahili kinapata hadhi.

**Maswali.**

(a) Bila kupoteza maana illiyokusudiwa na mwandishi, fupisha aya ya kwanza na ya pili. (maneno 50 - 60) (alama 6 utiririko 1)

(b) Kwa kuzingatia aya zilizobaki, eleza mambo muhimu anayoeleza mwandishi kuhusu ufundishaji wa Kiswahili katika vyuo vikuu. (maneno 60 - 70) (alama 9, utititiko1)

3. **SARUFI. (alama 40)**

(a) (i) Kimadende hutumkwa vipi. (alama 1)
(ii) Eleza sifa mbilimbili za sauti zifuatazo. (alama 2)
/d/
/m/

(b) Andika neno lenye silabi funge yenye muundo wa konsonanti moja. (alama 1)

(c) Onyesha matumizi ya "kwa" katika sentensi hii. (alama 3)
Kwa kuwa alikuwa mechelewa kwenda kwa nyanyake alisafiri kwa baiskeli.

(d) Tunga sentensi kwa kutumia. (alama 2)
(i) Kivumishi cha 'ki' ya mfanano.
(ii) Kielezi cha kiasi cha jumla.

(e) Baihisha shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo. (alama 4)
Kimathi alimwandikia babake bawa kwa kalamu jana jioni.

(f) Tunga sentensi ukitumia kitenzi cha katika hali ya kutendwa. (alama 1)

(g) Changanua sentensi hii kwa kutumia jedwali. (alama 4)
Mama alilima kwa bidii ingawa hakupta faida.

(h) Tunga sentensi moja yenye kishazi huru na kishazi kitegemezi ukitumia 'O' rejeshi tamati. (alama 3)

(i) Taja matumizi mawili mawili ya alama ifuatayo ya uakifishaji; (alama 2)
Mstari

(j) Andika sentensi ifuatayo kwa udogo wingi. (alama 2)
Mtu yule haachi kuandamana na mbwa wake aliyedhoofika kiafya.

(k) Andika katika msemo halisi. (alama 2)
Mwalimu alishangaa ni kwa nini Juma hakuwa amebaba mkoba wake siku hiyo.

(l) Kanusha sentensi hii katika hali ya 'a' (alama 2)
Kibofu hupa angani.

(m) Jibu kulingan ana maagizo. (alama 2)
(i) Ufisadi (unda kitenzi)
(ii) - pya (unda nomino)

(n) Andika maana mbili za neno "mlango". (alama 2)

(o) Tambua kinai kilichopigwa mstari katika senensi hii; (alama 1)
Watu <u>wenye woga mwingi</u> hukimbia ovyo.

(p) Mwanafunzi aliadhibiwa kwa uongo wake. (alama 2)
(Anza kwa .......Uongo)

(q) Andika kinyume. (alama 1)
Ukipitia kwao utalaaniwa.

(r) Andika upya sentensi hii kwa kutumia visuwe vya maneno yaliyopigwa mstri. (alama 2)
Lupita ndiye <u>alitakadamu upelelezi</u> wa shamba hili.

(s) Andika maana ya msemo. (alama 1)
Kawa na mihayara.

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479

4. **Isimu Jamii. (alama 10)**
(a) Kwa nini kulikuwa na haya ya kusanifisha lugha ya Kiswahili. (alama 5)
Toa sababu **tano**.
(b) Eleza sifa **tano** za sajili ya magazeti. (alama 5)

**MTIHANI WA MWIGO WA CEKENAS – 2016**
**KISWAHILI**
**102/3**
**KARATASI YA TATU**
**FASIHI**

**SEHEMU YA A**

**SWALI LA LAZIMA**

1. "Leo ndioyo mtanitambua. Mama gani anayemtazama mwana akigeuka afriti?"
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Tambua 'mwana aliyegeuka afriti'na ueleze hulka zake nne. (alama 6)
   (c) Jadili maudhui yoyote matano yanayojitokeza katika hadithi husika. (alama 10)

**SEHEMU YA B**
**Mtahiki Meya; Timothy Arege**
**Jibu swali la 2 au 3.**

2. "Siku moja kabla ya kufika kwa wageni. Meya ana mkutano na wawakilishi wa wafanyikazi ambao wameketi mkabala naye".

   (a) Fafanua madai yaliyotolewa na wafanyakzi katiak mkutano huu. (alama 12)
   (b) Eleza jinsi Meya alivyojibu madai ya wawakilishi wa wafanyakazi. (alama 8)

3. Tamthlia ya mstahiki Meya ni kioo cha jamii ya nchi za Afrika zinazoendelea. Thibitisha. (alama 20)

**SEHEMU YA C**
**Kidagaa kimemwozea.**
**Jibu swali la 4 au 5.**

4. Elimu ya kajielewa sisi nani, na twatoka wapi, twaelekea wapi na utu tutaurejeshaje pahali pake....
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Taja mfano mmoja wa tamathali ya usemi kwenye dondoo. (alama 2)
   (c) Dhihirisha jinsi utu ulivyotoka pahali pake, ukiregelea riwaya nzima. (alama 14)

5. Thibitisha kauli kuwa, "Mla naye huliwa zamu yake ifukapo'. Ukirejelea riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 20)

**SEHEMU YA D.**
**USHAIRI**
**Jibu swali la 6 au 7.**

6. **Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Angaza, mtazame mlimwengu
Bidii, nayo matokeo chungu
Wezesha, kuishi bila uchungu
Teknolojia maendeleo.

Angaza, zitazame barabara
Aenda, kwa kasi pia salama
Bidhaa, sokoni upesi fika
Teknolojia maendeleo.

Angaza, majokofu majumbani
Vyakula, na vinywaji hifadhika
Nafuu, zizima maji ridisha
Teknolojia maendeleo.
Angaza, leo pote madukani
Mikebe, vyakula vinywaji tiwa

for more free past papers visit: www.freekcsepastpapers.com or call: 0720502479